# Barazani

Jarida la **Baraza la Habari Tanzania**
Toleo la **186, Desemba, 2023**
ISSN **0856-874X**

*Kukuza Uhuru wa Vyombo vya Habari na kuhakikisha viwango vya juu kabisa vya weledi na uwajibikaji*




# Ndoto yatimia

**Pilikapilika za EJAT zaanza** Uk 5

**Nani kuwalinda waandishi?** Uk 11

**MAELEZO yakosoa** Uk 16



Katibu MKuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Dk. Peter Mathuki (kushoto) na Msemaji Mkuu wa Serikali ya Tanzania, Mohbare Matinyi wakifungua pazia kuonyesha nembo ya Baraza la Habari Afrika Mashariki (EAPC) katika uzinduzi wake Oktoba 19, 2023 kwenye makao makuu ya EAC Jijini Arusha.

MCT, MSHINDI WA TUZO YA IPI 2003 FREE MEDIA PIONEER



BODI YA UHARIRI:
Kajubi Mukajanga Katibu Mtendaji – MCT
Hamis Mzee Mhariri

MAWASILIANO
Kwa Maoni na Malalamiko:
Katibu Mtendaji
Baraza la Habari Tanzani (MCT)
S.L.P. 10160, Dar es Salaam
Simu: +255 22 27775728, 22 2771947
Simu ya Kiganjani: +255 784 314880
Fax: + +255 22 2700370
Baruapepe: media@mct.or.tz
Tovuti: www.mct.or.tz
Facebook:- www.facebook.com/mediacounciltanzania Twiter:- www.twitter.com/mctanzania

# EAPC ni hatua kubwa ya maendeleo

Kuzinduliwa kwa Baraza la Habari za Afrika Mashariki (EAPC) – chombo kinachojumisha mabaraza ya habari ya kanda hii ni hatua kubwa kwa maendeleo ya vyombo vya habari.

Wakati waanzilishi wake wakipata ahueni kwa kufanikisha ndoto yao,huu ni mwanzo wa kuimarisha maendeleo na ushrikiano wa vyombo vya habari katika nchi wanachama za Jumuia ya Afrika Mashariki.

Vyombo vya habari katika nchi za Afrika Mashariki vinafanyakazi katika mazingira tofauti. Katika baadhi ya nchi kuna mapigano ambapo kwenye nchi nyingine uhuru wa habari ni haba - hali hii itahitaji juhudi makini za pamoja kuwezesha kupatikana maboresho.

Kwa kuwa uzinduzi wake ulifanyika katika ukumbi wa Bunge la Afrika Mashariki, ni kielelezo kuwa ni mwanzo mzuri wa chombo hicho kipya cha wanataaluma ya habari.

Tunaamini mtazamo wa waanzilishi kuwa EAPC inazingtia ari na matakwa ya Jumuia ya Afrika Mashariki na inakumbatia tunu na malengo yake.

Ni kwa msingi huu ambapo EAPC iwe kichocheo ya hali nzuri kwenye vyombo vya habari na ichukue hatua kuhakikisha inafanikisha malengo yake ya kukuza na kulinda vyombo vya habari huru, vya kitaaluma na vinavyowajibika.

Ithibitishe kuwa siyo chombo kingine cha matamko tu cha kufurahisha wenye mamlaka ama chombo cha mkusanyiko wa "wanataaluma wachovu". Kichukue hatua kweli kufanikisha wingi wa vyombo habari na kujisimamia vyenyewe.

Uongozi wa EAPC udhihirishe imani waliyopewa kwa kutimiza malengo kama usemi kuwa "hakuna lisilowezekana".



Wawakilishi wa  nchi mbalimbali na waheshimiwa wakirusha njiwa kuashiria uzinduzi wa Baraza la Habari Afrika Mashariki(EAPC).

# Ndoto yatimia EAPC yazinduliwa

**Na Mwandishi wa Barazani**

"Ndoto imetimia", ndivyo Kajubi Mukajanga, Mwenyekiti wa chombo kipya cha usimamizi wa vyombo vya habari kwa nchi za Afrika Mashariki - Umoja wa Mabaraza ya Habari Afrika Mashariki (EAPC) alivyosema wakati wa uzinduzi wake Oktoba 19, mwaka huu.

Karibu wawakilishi 80 wa mabaraza ya habari, vyombo vya habari, wanahabari na wadau wa habari walikusanyika katika ukumbi wa Bunge la Afrika Mashariki katika makao makuu ya Jumuia ya Afrika Mashariki jijini Arusha kushuhudia tukio hilo la kihistoria.

EAPC, Mukajanga alisema, inazingatia dhamira na matakwa wa Jumuia ya Afrika Mashariki na malengo yake.

Alisema uongozi wa EAPC umeona ni muhimu kwa Umoja huo kuhusiana na Jumuia ya Afrika Mashariki kwa kuwa ni jumuia inayounganisha mataifa yote ya kanda hii.

EAPC ilisajiliwa rasmi nchini Kenya, Januari 20 mwaka huu.

Safari ya kufanikisha EAPC ilianza miaka minne iliyopita Oktoba 31, 2019 wakati viongozi wa Baraza la Habari la Kenya, Baraza la Habari la Uganda, Tume Habari ya Rwanda na Baraza la Habari la Tanzania walipokutana mjini Kisumu, Kenya na kuanzisha mchakato wa kuunda chombo cha kanda cha kutetea na kulinda uhuru wa habari.

Uongozi wa muda ulichaguliwa kwenye mkutano huo na ukandaa taratibu za chombo hicho na uamuzi ukachukuliwa wa kukisajili nchini Kenya ambapo sekretariati yake ilikuwa katika Baraza la Habari la Kenya.

Mkutano wa mtandao uliofanyika Arusha 2021 ulipitia na kukamilisha rasimu ya katiba ya umoja huo.

Kutokana na ushauri wa Katibu Mkuu wa EAC, Dk. Peter Mathuki, EAPC imeweza kujumuisha wanachama wengine toka nchi mbili – Congo DRC na Somalia. Matumaini yapo juu kwa Sudan Kusini na Burundi kujumuika na umoja huo.

Ujumbe wa uongozi wa EAPC – Mwenyekiti wake Mukajanga na David Omwoyo wa Baraza la Habari la Kenya ambaye ni Katibu wa umoja huo, ulikutana na Katibu Mkuu wa EAC Juni mwaka huu ambapo pamoja na kuuhakikishia ushirikiano wa Jumuia hiyo, aliwashauri kujumuisha pia nchi nyingine za Jumuia hiyo.

Lengo kuu la EAPC ni kukuza na kulinda vyombo vya habari huru vinavyowajibika katika kanda ya Afrika Mashariki na utaimarisha, kuhamasisha, na kukuza utaratibu wa vyombo vya habari kujisimamia kwa shabaha ya vyombo vya habari kuwajibika.

Katibu Mkuu wa EAC, Dk. Mathuki alijumuika na Mkurugenzi wa Idara ya Habari na Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi aliyemwakilisha Waziri Nape Nnauye, kufungua pazia la nembo ya EAPC na

*Endelea Ukurasa wa 4*

# Ndoto yatimia EAPC yazinduliwa

*Inatoka Ukurasa wa 3*

baadaye wakaungana na viongozi waandamizi wa Umoja huo kurusha njiwa weupe ikiwa ni ishara ya uzinduzi huo.

Katika hotuba ambayo aliisoma kwa niaba ya Katibu Mkuu wa EAC, Dk. Irene Isaka, Mkurugenzi wa Sekta za Jamii katika Jumuia alieleza matumaini ya Katibu Mkuu kwamba kuanzishwa kwa EAPC kutawezesha kuwepo vyombo vya habari huru vitakavyokuza misingi ya demokrasia, haki ya jamii na kuheshimu haki za binadamu katika kanda nzima ambayo sasa imepanuka kutoka pwani ya mashariki hadi ya magharibi mwa Afrika.

Dk. Mathuki alisema kuwa uandishi wa habari huru wenye weledi ni msingi wa uendelezaji wa demokrasia ambapo ukikosekana uhuru wa habari unaathirika, na pia haki za msingi za jamii.

"Vyombo vya habari vilivyochangamka ni muhimu kwa kufanikisha haki za kijamii, utawala wa sheria, uwajibikaji, usawa na kulinda kwa haki za binadamu. Jamii inaathirika kama vyombo vya habari havifanyi kazi yake kwa uhuru na weledi kwa kuwa njia za kujieleza kwa uhuru zitakuwa zimebinywa na habari za maslahi ya umma kutopatikana, ikiwamo kudorora kwa uandishi wa habari za uchunguzi," alisema Katibu Mkuu wa EAC.

"Bila uandishi huru, jamii na hasa makundi dhaifu wakiwamo wanawake na vijana, wanaathirika kwa kuwa hawana njia wala taarifa muhimu kuwawajibisha viongozi na kudai wanachostahili ," aliongeza Dk. Mathuki.

Kwa upande wake, Matinyi – Mkurugenzi wa Idara ya Habari na Msemaji Mkuu wa Serikali ya Tanzania amevitaka vyombo vya habari kutumia teknolojia mpya kuelimisha na kuwahabarisha wananchi kuhusu masuala muhimu muhimu kwao, ikiwa ya utamaduni, siasa na uchumi.

Matinyi akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Habari , Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Moses Nnauye, alisema vyombo vya habari vinapitia mabadiliko yasiyoepukika kutokana na kukua kwa teknolojia.

Alieleza matumaini kwamba EAPC, na mabaraza ya habari ya nchi za Afrika Mashariki



*Dk. Irene Isaka, Mkurugenzi wa Sekta za Jamii katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), akisoma hotuba ya uzinduzi wa Baraza la Habari la Afrika Mashariki, kwa niaba ya  Katibu Mkuu wa (EAC)  Dk. Peter Mathuki.*

yatabadilishana uzoefu na kushauri serikali zao jinsi ya kufanikisha malengo ya kuwa na vyombo huru vya habari vinavyozingatia weledi, maadili, kuwajibika, na uzalendo.

Katibu wa EAPC na Mtendaj Mkuu wa Baraza la Habari la Kenya, David Omwoyo Omwoyo, amehimiza kutumika kwa viwango sawa kwa vyombo vya habari katika kanda kuwezesha kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi.

Mweka Hazina wa EAPC na Katibu Mtendaji wa Tume ya Habari ya Rwanda, Emmanuel Mugisha, amesema Rwanda imekuwa ikitumia vyombo vya habari kuhakikisha vijana na umma kwa jumla wanaandaliwa vizuri kutumia vyombo vya habari hasa fursa za mtandaoni kwa umakini.

Katika uzinduzi huo mjadala ulifanyika kuhusu masuala mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ya teknolojia katika uandishi wa habari.

Mjadala huo uliratibiwa na Joe Ageyo wa Nation Media Group ya Kenya, ambapo washiriki walikuwa Emmanuel Mugisha wa Tume ya Habari ya Rwanda , Peter Okello kutoka Baraza la Habari la Uganda, Linus Kaikai wa Royal Media Services , Kenya , Nuzulack Dausen wa Nukta Africa ambaye pia ni mwandishi wa Thomson Reuters, na Anastazia Rugaba na Twaweza Afrika Mashariki.

# Pilikapilika kuwania EJAT 2023 zaanza

Na Mwandishi wa Barazani

Pilikapilika na heka heka za kuwania Tuzo za Umahiri katika Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) zinazolenga kuwatambua na kuwatuza waandishi wa habari zimeanza kufuatia kuzinduliwa rasmi Tuzo hizo Novemba 15, jijini Dodoma.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya EJAT, Kajubi Mukajanga, alizindua Tuzo hizo ambazo safari hii zitakuwa na makundi mawili mapya - Habari za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Habari za Malezi na Makuzi ya Awali ya Mtoto.

Kwa mujibu wa waandaaji, makundi haya yameongezwa ili kushajiisha ubora wa uandishi habari katika maeneo hayo.

Pamoja na nyongeza ya makundi hayo, makundi ya Habari za Sayansi na Teknolojia; na Habari za Sensa yameondolewa katika orodha ya makundi yatakayoshindaniwa katika Tuzo hizo kutokana na mwitikio mdogo wa uwasilishaji kazi kutoka kwa waandishi wa habari na kukosekana kwa ufadhili wa uhakika.

Hata hivyo, waandishi wenye habari za maeneo haya ambao wanaona kazi zao ni nzuri wamehimizwa kuziwasilisha kupitia makundi mengine kama Uchumi, Biashara na Fedha, au Elimu, au Kundi la Wazi na kundi la Habari za Gesi, Mafuta na uchimbaji madini kutegemea na watakavyoshauriana na wahariri wao.

Hii itakuwa ni mara ya 15 kwa Kamati ya Maandalizi ya EJAT ikiongozwa na MCT kuandaa mashindano haya mfululizo bila kukosa, ambapo kwa mara ya kwanza yalifanyika mwaka 2009.

Kufuatia uzinduzi huo waandishi wa habari wa magazeti, radio, runinga na vyombo vya habari vya mtandaoni wametakiwa kuanza kuwasilisha kazi zao zilizochapishwa au kutangazwa mwaka huu.




*Mshindi wa jumla wa Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) 2022, Sanula Athanas katikati akiwa ameshikilia mfano wa hundi ya sh. milioni tatu aliyokabidhiwa na Mgeni rasmi, Katibu Mkuu Kiongozi Ombeni Sefue (kushoto).*

Utaratibu wa kuwasilisha kazi utakuwa wa aina mbili: kwa njia ya mtandao au kwa kuwasilisha fomu ambayo inapatikana kwenye tovuti ya MCT ya www.mct.or.tz.

Makundi yanayoshindaniwa ni kama ifuatavyo:- Tuzo ya Uandishi wa Habari za Uchumi, Biashara na Fedha; Tuzo ya Uandishi wa Habari za Michezo na Utamaduni; Tuzo ya Uandishi wa Habari za Kilimo na Biashara ya Kilimo; Tuzo ya Uandishi wa Habari za Elimu na Tuzo ya Uandishi wa Habari za Utalii na Uhifadhi.

Mengine ni Tuzo ya Uandishi wa Habari za Uchunguzi; Tuzo ya Uandishi wa Habari za Data;Tuzo ya Uandishi wa Habari za Haki za Binadamu na Utawala Bora;Tuzo ya Uandishi wa Habari za Jinsia na Watoto; Tuzo ya Uandishi wa Habari za Walemavu; Tuzo ya

Endelea Ukurasa wa 6

# Pilikapilika kuwania EJAT 2023 zaanza

*Inatoka Ukurasa wa 5*

Uandishi wa Habari za Afya;Tuzo ya Uandishi wa Habari za Ushirika na Tuzo ya Uandishi wa Habari za Kodi, Tozo na Mapato.

Mengine ni Tuzo ya Uandishi wa Habari za Hifadhi ya Jamii; Tuzo ya Uandishi wa Habari za Utunzaji wa Mazingira na Vyanzo vya Maji;

Tuzo ya Uandishi wa Habari za Afya ya Uzazi; Tuzo ya Uandishi wa Habari za Malezi na Makuzi ya Awali ya Mtoto; Kundi la Wazi; kundi la Habari za Gesi, Mafuta na uchimbaji madini.

Washindi katika makundi hayo mbalimbali huzawadiwa Tuzo, vyeti, fedha taslim na zawadi zingine.

MCT pia hutoa udhamini wa masomo wenye thamani ya shilingi za Kitanzania milioni tatu kwa mshindi wa jumla ili ajiendeleze kitaaluma katika masuala ya uandishi wa habari kulingana na mahitaji yake.

Imeelezwa pia kuwa mwaka huu, Tuzo ya Mshindi wa Maisha Katika Uandishi wa Habari (LAJA), ambayo hutolewa mwandishi aliyetoa mchango mkubwa katika kuimarisha taaluma ya uandishi wa habari na uhuru wa vyombo vya habari , itaendelea kutolewa na hii itakuwa mara ya nane.

Waandishi nguli waliowahi kupata tuzo hiyo ni pamoja na marehemu Fili Karashani (2012), Hamza Kassongo (2013), Mariam Hamdani (2014), Jenerali Ulimwengu (2015), Rose Haji (2016),Ndimara Tegambwage (2022)na Tido Mhando (2023).

Tamasha la (EJAT) 2023 limepangwa kufanyika Julai 27, 2024 katika ukumbi ambao utatajwa baadaye. Mwisho wa kuwasilisha kazi za waandishi ni Januari 31,2024.

Katika EJAT 2022 ambayo kilele chake ilikuwa Julai 22, 2023 kazi 893 ziliwasilishwa kuwania Tuzo hizo kulinganisha na kazi 598 za mwaka uliopita ikiwa ni ongezeko la asilimia 49.

Katika kuandaa Tuzo hizi, MCT inashirikiana na wadau wengine wa habari wakiwamo Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika- Tawi la Tanzania (MISA-Tan), Wakfu wa Vyombo vya Habari Tanzania (TMF), Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Chama Cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA),Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC) na HakiElimu.




*Wawakilishi wa wafadhili mbalimbali wa Tuzo za Umahiri za Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) 2022 wakiwa na vyeti vyao katika picha ya pamoja na Mgeni rasmi wa tuzo hizo, Katibu MKuu Kiongozi mstaafu Ombeni Sefue ( wa saba kutoka kulia) na Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Tuzo hizo, Kajubi Mukajanga ( wa sita kutoka kushoto).*




Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Baraza la Habari Tanzania, Nico Mwaibale kutoka Uyui FM ya Tabora ambaye alikuwa Mwenyekiti wa uchaguzi wa wajumbe wa bodi ya Baraza akipiga kura.

# Mjadala wa kitaifa kuhusu uchumi wa vyombo vya habari wapangwa

**Na Mwandishi wa Barazani**

Baraza la Habari Tanzania (MCT) kwa kushirikiana na wadau limepanga kuanzisha mjadala wa kitaifa kuhusu hali ya uchumi ya vyombo vya habari.

Akiwasilisha ripoti ya utekelezaji ya shughuli za Baraza katika Mkutano Mkuu wa 25 wa Baraza uliofanyika Arusha Septemba 28,2023, Katibu Mtendaji wa MCT, Kajubi Mukajanga alisema wakati mazingira ya kisheria na kiusimamizi yanaendelea kuwa bora zaidi, hali ya uchumi wa vyombo vya habari inakuwa mbaya.

Alisema vyombo vingi vya habari viko katika hali mbaya kiuchumi na kuathiri siyo tu uwezo wao wa kuwekeza kukuza maudhui bora na ya kiuchunguzi bali pia kuwalipa vizuri watumishi wao.

Suala la uchumi wa vyombo vya habari ni miongoni mwa mambo muhimu yaliyomo kwenye mpango mkakati wa Baraza wa mwaka 2023 hadi 2027 uliopitishwa na Bodi ya Baraza Desemba 2022.

Mpango mkakati huo ambao Baraza limeanza kutekeleza Januari mwaka huu unajumuisha maeneo manne ambayo ni pamoja na uchechemuzi wa sera na sheria, uhuru wa habari na usalama wa waandishi wa habari, maadili na usuluhishi mbadala pamoja na maendeleo ya vyombo vya habari na ufuatiliaji.

Kuimarisha na kuboresha shughuli za vyombo vya habari ni lengo kuu la mpango mkakati huo.

Akizungumzia kupungua kwa matukio ya ukiukwaji wa uhuru wa habari, Mukajanga alisema hii haimaanishi kwamba matatizo yameisha, akieleza kuwa yapo matukio yameripotiwa kwa mwaka huu na kurekodiwa katika kanzi data ya Baraza.

Akizungumzia marekebisho ya sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari yaliyopitishwa na Bunge Juni, mwaka huu, Mukajanga alisema jitihada za wadau zimezaa matunda.

Ingawa siyo mapendekezo yote ya wadau yalijumuishwa licha ya ahadi nzuri za serikali, alisema,

*Endelea Ukurasa wa 11*

# JINSI YA KUWASILISHA MALALAMIKO MCT

- Taasisi au mwananchi anayehisi kukosewa na chombo cha habari ambacho ni gazeti, redio, runinga ama cha kimtandao anashauriwa kuwasilisha malalamiko yake Sekretariati ya Baraza la Habari Tanzania.
- Mlalamikaji anaweza kuwasilisha malalamiko yake kwa njia ya:
- Simu
- Barua
- Barua pepe
- Fomu maalumu inayopatikana kwenye tovuti ya Baraza ambayo ni mct.or.tz
- Malalamiko hayo yaainishe sababu ya malalamiko yake, jambo analoomba Baraza limfanyie kuhusiana na malalamiko yake pamoja na ushahidi wowote alionao.
- Mlalamikaji awasilishe malalamiko yake haraka iwezekanavyo na kwa namna yoyote ile isizidi miezi sita tangu siku yalipochapishwa au kutangazwa.
- Malalamiko yatashughulikiwa na kukamilika katika muda usiozidi miezi mitatu baada ya kupokelewa.

Maamuzi ambayo Baraza linaweza kutoa

- Ni kama mlalamikiwa amekosa au la.
- Kumtaka mlalamikiwa kumwomba radhi mlalamikaji.
- Kumtaka mlalamikiwa kusahihisha habari inayolalamikiwa.
- Kumtaka mlalamikiwa kumpa mlalamikaji haki ya kujibu.
- Kumtaka mlalamikiwa kulipa gharama halisi alizotumia mlalamikaji kuhusiana na shauri linanalolalamikiwa.

Kama mlalamikaji hakuridhika na upatanishi wa Kamati ya Maadili ya Baraza la Habari Tanzania ana haki ya kupeleka malalamiko yake mahakamani. Hata hivyo taarifa za mwenendo wa usuluhishi ndani ya Kamati hazitatolewa mahakamani kama sehemu ya ushahidi. Baraza pia halitapokea na kusikiliza shauri ambalo lipo mahakamani.
Tafadhali bonyeza hapo chini kwa taarifa zaidi

**USULUHISHI WA MALALAMIKO**

Baraza la Habari Tanzania (MCT)
S.L.P 10160, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22-2775728/2771947
Mob: +255 719 494640/686 494640/767498426
Barua pepe: media@mct.or.tz
Tovuti: www.mct.or.tz


Waandishi wa habari wakiwa kazini.

# Serikali yahimizwa kuandaa mazingira rafiki kwa wananahabari kufanya kazi

Na Mwandishi wa Barazani

Serikali imehimizwa kutengeneza mazingira rafiki ya utendaji kazi kwa waandishi wa habari ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa taarifa pamoja na uhuru wa kujieleza kwa wananchi, taasisi na vyombo vya habari.

Katika taarifa ya kuadhimisha siku ya kimataifa ya kupinga ukatili dhidi ya waandishi wa habari – International Day to End Impunity for Crimes against Journalists (IDEI) ambayo huadhimishwa kila tarehe 2 Novemba – Baraza la Habari Tanzania (MCT) limeitaka serikali:

- Kuwachukulia hatua wale wote wanaozuia ama kukwamisha utendaji kazi wa waandishi wa habari katika upatikanaji wa taarifa katika ofisi za umma kinyume cha sheria;
- Kusimamia suala la upatikanaji taarifa kwa haraka na kwa usahihi, na kuhakikisha wakurugenzi wa halmashauri za wilaya wanatimiza maelekezo ya Waziri Mkuu. Aliziagiza Wizara, Taasisi za Umma na Idara za Serikali kutenga bajeti kwa ajili ya kugharamia shughuli za utoaji taarifa kwa wananchi, kwa usahihi na kwa haraka; na
- Kuwawekea mazingira salama ya kufanya kazi zao waandishi wa habari na kuwafikisha mahakamani wale wanaofanya uhalifu dhidi ya waandishi.

Kwa waandishi wa habari Baraza limewataka:-

- Kufanya kazi kwa weledi mkubwa, kufuata maadili na miongozo ya uandishi wa habari katika kazi zao za kila siku;
- Kuchukua tahadhari hasa ya mabadiliko ya teknolojia ili kuepukana na taarifa za uongo; na
- Kuendelea kusaka taarifa kwa kufuata sheria inavyoelekeza.

Ambapo kwa jamii limehimiza:-

Wananchi kuomba taarifa mbalimbali katika maeneo yao ili kupata haki zao, na pale wanapo nyimwa taarifa, wasisite kuripoti katika taasisi husika juu ya jambo hilo.

Taarifa ya MCT kuadhimisha IDEI iliyosainiwa na Katibu Mtendaji wa Baraza , Kajubi Mukajanga iliyotolewa akiwa katika ziara mkoani Lindi imeeleza pia Baraza limebaini kuwa bado kuna tatizo katika utoaji wa taarifa na kuwa pamoja na maelekezo ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa aliyoyatoa Machi 27, 2023 katika kikao kazi cha 18 cha maafisa habari, uhusiano na mawasiliano wa umma, kilichofanyika jijini Dar es Salaam, matukio ya wanahabari kunyimwa taarifa yanaongezeka.

Waziri Mkuu aliziagiza Wizara, Taasisi za Umma na Idara za Serikali kutenga bajeti kwa ajili ya kugharamia shughuli za utoaji taarifa kwa wananchi, kwa usahihi na kwa haraka.

Mbali na kukiukwa kwa agizo la Waziri Mkuu, taarifa hiyo imesema baadhi ya maafisa wanatoa maamuzi ambayo yanakwenda kinyume na sheria ya Haki

Endelea Ukurasa wa 14



Wananachi wakiwa kwenye kituo cha kupiga kura kutimiza haki yao ya kikatiba ya kuchagua viongozi wao wanaowapenda.

# Nani kuwalinda waandishi wakati wa uchaguzi ?

**Na Tumbi Kiganja**

Mei 3 mwaka huu Baraza la Habari Tanzania (MCT) lilitoa taarifa ya madhila yaliyowakumba waandishi wa habari kwa kipindi cha miaka kumi (10) iliyopita, ambapo jumla ya wanahabari 272 na vyombo vya habari 94 vilikumbwa na madhila mbalimbali.

Taarifa hiyo ya MCT ilielezea madhila yaliyowasilishwa kuanzia mwaka 2012 hadi mwaka 2022 ambayo yalikuwa kwenye sura ya kunyimwa taarifa, kutishiwa, kukamatwa, chombo cha habari kufungiwa, kutekwa nyara, kuingiliwa kwa uhuru wa uhariri, faini kwa chombo cha habari, vifo, kuharibiwa vifaa vya kazi, kuondolewa katika eneo la tukio kinyume cha sheria na kujidhibiti .

Kwa mujibu wa MCT, taasisi na mamlaka za Serikali ndizo ziliongoza kwa kuwafanyia waandishi wa habari madhila hayo, zikiongozwa na jeshi la polisi lililohusika na matukio 51, huku Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) matukio 21, Wizara mbalimbali matukio 14, wakuu wa wilaya matukio tisa.

Jeshi la polisi ndiye mlinzi wa raia na mali zake. Kuwa mwandishi wa habari haiondoi ile haki yako ya kuwa raia, hivyo na wao wanapaswa kupata ulinzi kama raia wengine wa Tanzania na hata vitendea kazi vyao pia kulindwa na jeshi hilo; lakini je kwa mujibu wa takwimu hizi tunaweza kusema kuwa jeshi la polisi lilitimiza wajibu wake namba moja kwa kundi hili la raia wa Tanzania?

Serikali ndiye baba na ndiye mama wa wananchi wa taifa husika, TCRA, wizara, wakuu wa wilaya hizi zote ni mamlaka za Serikali ambazo tunaratajia ndiyo ziwe za kwanza kuwapa ushirikiano waandishi wa habari kwa kuwa ndiyo wamekuwa wakiwatumia ili kupeleka ajenda zao kwa wananchi kwa kupitia vyombo vya habari.

Kulingana na takwimu hizi, itakuwa sahihi nikisema kuwa bado jeshi la polisi na baadhi ya mamlaka nyingine za Serikali hazitimizi wajibu wake vile inavyotakiwa katika kutoa ushirikiano na ulinzi kwa waandishi wa habari.

Mwaka 2024 na 2025 nchi yetu inaelekea kwenye chaguzi, uchaguzi wa serikali za mitaa na hatimaye

*Endelea Ukurasa wa 11*

# Mjadala wa kitaifa kuhusu uchumi wa vyombo vya habari wapangwa

*Inatoka Ukurasa wa 7*

inatia moyo kwamba marekebisho yamefanyika.

Pia alisema kuna mwelekeo chanya katika mchakato wa kupata sheria mpya ya habari Zanzibar.

Alisema hii inatokana na ahadi ya Rais Dk. Hussein Mwinyi aliyoitoa alipokutana na ujumbe wa MCT Desemba mwaka jana aliyoirudia alipokuwa mgeni rasmi wa maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Habari mjini Zanzibar mwezi Mei.

Mwezi Septemba 2023 Waziri wa Habari wa Zanzibar, Tabia Maulid Mwitta aliwaambia wadau wa habari pamoja na MCT kwamba muswada sheria mpya ya habari umekamilishwa na sasa unatafsiriwa kwa Kiingereza, Mukajanga alisema.

Alisema kuwa kuna mwanga mpya kwa sababu ahadi ya kubadili sheria imetolewa na serikali yenyewe.

Hata hivyo alionya kuwa wasibweteke bali waichukulie hatua hiyo kuwa mwito wa kuongeza jitihada kubadili sheria zingine.

Kikanda, Mukajanga alisema kumekuwa na maendeleo mazuri kwamba mabaraza ya habari ya Rwanda, Tanzania, Kenya na Uganda yameanzisha na kusajili Chama cha Mabaraza ya Habari ya Afrika Mashariki ambapo yeye ndiye Mwenyekiti .

Amefahamisha kuwa nchi mbili za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Somalia zimejiunga katika chama hicho.

Mukajanga pia alisema kwenye mkutano huo kuwa wanachama wapya 12 wamejiunga na MCT kufanya idadi ya wanachama kuwa 243.

Wanachama hao wapya waliotambulishwa rasmi katika mkutano huo mkuu wa MCT ni The Chanzo, Chuo Kikuu cha Zanzibar, Radio Uhai, Runinga ya jamii ya Sunet ya Zanzibar , Chuo Kikuu Huria Tanzania , Mtolera Limited , Media Aid for indigenous Pastoral Communities (MAIPAC), Kilimanjaro Revival FM, Harvest Time na El Olama FM Radio. ,

# Nani kuwalinda waandishi wakati wa uchaguzi ?

*Inatoka Ukurasa wa 10*

uchaguzi mkuu. Wote tunaelewa kuwa nyakati za uchaguzi ndipo kunakuwa na changamoto nyingi sana ambazo huwakuta waandishi wa habari kwani vyama na wagombea hutarajia vyombo na waandishi wa habari kuwa upande wao daima na pindi inavyokuwa tofauti basi ghafla uadui huibuka.

Hivi jamii inajua kuwa uandishi wa habari ni taaluma? Tena inayofanya kazi kwa kuongozwa na maadili, misingi waliojiwekea hasa kusimama kwenye mstari mnyoofu na kukemea yale machafu yote kwa manufaa ya jamii husika?

Jua bado lingali latoa mwangaza, hivyo shime waandishi wa habari anzeni kujipanga mapema kabla ya 2024.

Ndugu zangu waandishi hebu rejeleeni kwenye Mwongozo wa Waandishi wa Habari Kuripoti Uchaguzi Tanzania (Reporting Elections in Tanzania) ambao ulichapishwa na MCT kwa mara ya kwanza mwaka 2009 na kuchapwa mara ya pili mwaka 2010

Mwongozo huu tukiusoma na kuufanyia kazi utatusaidia kutupunguzia misuguano baina yetu na wanajamii ambao wanajifanya hawaoni umuhimu wetu au kudharau kile tunachokifanya lakini wakitaka kupeleka ujumbe wao wanatuita tena kwa kupiga simu mara mbilimbili kwenye vyumba vyetu vya habari: “Samahani Ndugu Mhariri….mimi ni Ndumilakuwili napiga simu kutoka Ofisi ya mwenye madaraka anaeweza kufanya sukari ikawa chumvi. Naomba waandishi wako watatu tena naomba wenye uwezo wa kupiga picha na kuandika habari nzuri itayotuuza”

Pamoja na mambo mengi yaliyoelezewa na kuchambuliwa ndani ya Mwongozo huu, mwandishi atajifunza pia kuelewa ni namna gani suala la maadili anapaswa kulizingatia wakati wa kuripoti uchaguzi, namna gani ya kujiandaa na kujilinda kabla na wakati anapokwenda kwenye kampeni za vyama vya siasa. Aidha mwandishi anapaswa kufany

a uchunguzi wa namna gani wakati anafanya habari hizi za uchaguzi na kadhalika.

Mambo haya machache na mengine mengi yaliyozungumziwa katika Mwongozo huu yatamsaidia mwandishi wa habari kujilinda na kepukana na madhila yasiyo ya lazima kwake.

Nakumbuka mwandishi mkongwe na Mshindi Tuzo ya Mafanikio ya Maisha (LAJA) 2011 inayotolewa na MCT, Marehemu Fili Karashani aliwahi kusema kuwa wananchi wanahitaji kupata habari toka kwa waandishi wa habari hivyo ni muhimu kumlinda na kujali usalama wako kama mwandishi wa habari. “Usife kwa ajili ya habari kisha wewe ndio ukawa habari,” alisisitiza.

# Wasemavyo wafanyakazi kuhusu Mukajanga

**Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Kajubi Mukajanga, anastaafu mwishoni mwa Desemba 2023 baada ya kulitumia Baraza hilo kwa miaka 15. Wafanyakazi wa Baraza hilo wanaelezea uongozi wake na alikuwa ni mtu wa aina gani. Endelea...**

## Paul Mallimbo



Mzee Kajubi ni mtu ambaye amenisaidia sana kujitambua katika utendaji wangu wa kazi. Ni mtu makini linapokuja suala la kazi hana mzaha wala urafiki. Huyu mzee ukifanya naye kazi ukashindwa kukua kitaaluma utakuwa na tatizo ambalo linahitaji msaada nje ya hali ya kawaida ya kibinadamu.

Ni mwalimu wa lugha zote mbili Kiingereza na Kiswahili. Anapenda watu wajifunze, unajua huyu mzee ni Mchapishaji , mimi amenifundisha mambo ya Ukurasa wa Hakimiliki, sikuwahi kuyajua, lakini pia amenifundisha namna ya kuweka Namba za Kurasa za Vitabu, mambo ya Namba zinazogawanyika na zile zisizogawanyika ambayo sikuwahi kujua kabla ya kuingia MCT.

Kajubi ni mtu makini, ni mtu ambaye hata jina lako ukilikosea hatakuacha salama. Kuna mfanyakazi mwenzangu aliwahi kuandika jina la aliyekuwa Mkurugenzi wa Masoko wa TBC1 Eliza, badala ya Elizabeth, hakumuacha salama alimpa vidonge vyake na kumhimiza kuwa makini katika kuandika majina ya watu.

Kajubi Mukajanga ni mhariri, ukiandika nyaraka yako ukampatia, akaipitia akiirudisha utapenda, kwa maana nyaraka yako inakuwa imeandikwa kwa lugha fasaha inayoeleweka.

Kajubi ana msimamo na akisimamia jambo fulani ni lazima liwe tena kwa kiwango cha juu, ni mtu asiyependa kufanya kitu katika viwango hafifu au vya chini. Ni mtu wa viwango.

Ni kiongozi mwenye kulenga kwa usahihi vipi na namna anataka afanikiwe kwa kila anachokifanya au kukifikiria.

Kuhusu masuala ya maadilio ya sharia kwa vyombo vya habari, utaona ni yeye ndiye aliyeanzisha na kusimamia mchakato mpaka ukafika hapo ulipo. KM ni kiongozi ambaye anasikiliza ushauri kutoka kwa wasaidizi wake kabla ya kufanya maamuzi yoyote yanayohusu taasisi au jambo lenye maslahi mapana kwa tasnia ya habari.

Pamoja na hayo yote Kajubi ni mkali, ukitaka kufanya naye kazi hakikisha miongozo ambayo mmejiwekea, na hapa nazungumzia mpangokazi, inafuatwa kadiri mlivyojipangia, nje ya hapo hamtaelewana. Ni mtu anayependa matokeo yanayohitajiwa yanapatikana au hata ikibidi malengo yanavukwa.

Ukiangalia baadhi ya mambo ambayo katika uongozi wake, ni kwa sababu ya umakini wake na kuwa mtu wa matokeo chanya. MCT sasa hivi ina jengo lake, na pia inaendelea kujenga ofisi zake za kudumu pale Tegeta Skanska. Hili ni mojawapo ya matunda ya KM wakati wa uongozi wake. Litakuwa jambo la busara sana iwapo hilo jengo likikamilika likaitwa Kajubi Tower, Kajubi Media House au Kajubi Mukajanga Media Tower.

## CPA Mustafa Tarimo



Kajubi amekuwa ni kiongozi bora, mshauri mzuri na rafiki mwema. Ushauri wake umenisaidia sana kujiendeleza kitaluma na kibinafsi. Wakati wote tupo pamoja naye kupeana taarifa muhimu na ushauri katika timu yetu. Tunashukuru na kufurahi kwa kuwa na kiongozi kama huyu. Binafsi natoa shukrani kwa kupata nafasi ya kufanyakazi na Katibu Mtendaji aliye bora.

## Bertha Christopher



Ni kiongozi mzuri na pia ni mwalimu. Mimi nimejifunza vitu vingi chini ya uongozi wake ikiwa pamoja na kuwa na taratibu na mpangilio mzuri wa kufanya kazi. Kwa kweli amenishape kufanya kazi zangu vizuri kiofisi. Amekuwa makini katika kuandaa mpango kazi kiasicha kumfa kila mmoja wetu kujua amajukumu yake na anachotakiwa kwa mpangilio. Mikutano ya quarter planning imessaidika katikakuweka sawa utendaji kazi.

Kwa jumla nikiongozi mzuri. Nimenufaika na uongozi wake.

## Tumbi Kiganja



KAJUBI MUKAJANGA

Binafsi MCT ndio mahala pangu pa kwanza kabisa kufanya kazi nikitokea chuoni. Wakati naingia MCT nilikuta Kajubi Mukajanga akiwa Katibu Mtendaji wa MCT na ndie aliyenipokea kwa wakati huo. Kajubi ana sifa nyingi kiutendaji ambazo hata kama nitazielezea hapa sitaweza kuzimaliza lakini Kajubi ni kiongozi wa aina yake, ni Mwalimu pia ambaye anauweza mkubwa wa kumtengeneza mwandishi wa habari mchanga na kuwa mwandishi habari makini. Kwa upande wa Uongozi Mungu amemjaalia kipawa cha aina yake

**Pia Kajubi ni**

1. Kiongozi mzuri anaeweza kuifanya Taasisi na wafanyakazi wake wakashikamana na kufanya kazi kwa umoja na mshikamano,
2. Ni kiongozi anayejua na kuthamini na kuimarisha mawasiliano Ndani ya Taasisi

Anatoa nafasi ya kulea na kusikiliza wafanyakazi wake na kuwapa nafasi ya kukua.

## Shiffaa Said Hassan



Mambo muhimu katika uongozi wa Kajubi Mukajanga.

Aliimarisha ofisi yetu ya Zanzibar kwa kuwa na programme maalum na mpango kazi ambao ulikuwa ni dira ya kuimarisha shughuli za Baraza la Habari katika visiwa vya Unguja na Pemba.

Kuliandikwa vitabu ya historia ya Vyombo vya Habari Zanzibar pamoja na tafiti mbalimbali za uwanda wa vyombo vya habari Zanzibar ambazo zimekuwa ni hazina ya kujivunia katika kuweka kumbukumbu nzuri na kuwa ni moja ya vitabu ambavyo vimekuwa vikifuatiliwa sana na waandishi wa habari pamoja na wanaojiendeleza katika taaluma ya habari.

Kuwepo na Media Resource centre ambayo imesheheni vitabu muhimu vya tasnia ya habari ambavyo vimekuwa ni faraja kwa wanafunzi na waandishi wa habari kwa kufanya references mbali mbali.

Nimejifunza usimamizi wa muda katika kazi lakini pia ripoti ambazo sio tu zinaonyesha kufanyika kwa shughuli bali pia zinaonyesha matokeo ya pamoja na kuweza kuweka kumbukumbu vizuri za mafanikio baada ya kila shughuli na changamoto zilziojitokeza.

Umuhimu wa kuwa na mpangokazi katika kila mwaka na kwa kila robo mwaka ili kuwa na dira ya shughuli zitakzofanyika kwa wakati.

Kufuatilia kwa karibu uhuru wa habari Zanzibar katika masuala mawili makuu suala la maaadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Habari duniani na kufanyika Zanzibar kwa ukubwa wa kitaifa na pia kufuatilia kwa karibu masuala ya mabadiliko ya sheria za habari na umuhimu wa kuwa na sheria nzuri za habari.

Suala la jinsia na vyombo vya habari limepewa kipaumbele na kuwepo kwa programme maalum katika eneo hilo mathalan tulianza na utafiti wa jinsia na vyombo vya habari, tukawa na sera ya jinsia na vyombo vya habari, tukawa na mafunzo ya wanawake na uongozi katika vyombo vya habari lakini pia kuanzisha kwa madawati ya jinsia katika vyombo vya habari.

Kufuatilia vyombo vya habari hususan katika masuala ya taaluma na maadili na masuala mengine kama jinsia, watoto, na walemavu.Hapa pia nimejifunza kufuatilia mwenendo wa vyombo vya habari na kuandika ripoti pamoja na kufuatilia.

Hayo ni baadhi ya mambo ambayo nimejifunza kutoka kwa Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania. lakini pia la muhimu zaidi nikiwemo kwenye menejimenti ni kwa namna gani aljiitahidi katika kuwa na maamuzi ya pamoja na kujali maoni wa wajumbe wa menejimenti na kupingana kwa hoja. Shukuran.

## Saumu Mwalimu

**Kajubi wa Miaka yangu 7 na MCT**

Ni furaha kupata nafasi ya kufanya kazi na wewe, kwangu MCT sio tu sehemu ya kazi lakini ni chuo kikuu. Uwezo wako wa kuhakikisha, ninajifunza kazi aina mbalimbali mbali na zile zilizo kwenye adidu rejea za mkataba wangu umenipa nafasi ya kuwa na ujuzi tofauti tofauti.

Una nguvu kubwa sana ya kuunganisha watu, sio tu MCT lakini hata katika makundi mengine, MCT imekua familia inayojaliana si-tu wakati wa kazi bali hata nje ya kazi na hii ni hata kwa maeneo mengine, CoRI kwa mfano, umetufanya kuwa ndugu na ikaturahisishia sana utendaji wetu wa kazi.

Umakini. Hapa nimejifunza jambo kubwa sana. Umakini katika kila kitu



hata kama kinaonekana kidogo, hii imetusaidia sana nyaraka zetu kuwa bora na sasa umetuachia msingi imara sana.

Kusikiliza na kutoa nafasi. Hili nitalipeleka hata nyumbani kwangu. Kwako hakuna mwenye kujua zaidi ya mwingine, wote ulitupa nafasi ya kusikilizwa na kutoa maoni huku ukisisitiza kufanya kazi katika timu wakati huo huo tukijitisimamia wenyewe.

Ushawishi. Hapa nakuvika taji. Ukisema, imetosha. Ujuzi wako wa kupangilia maneno ya kusema ama kuandika na ushawishi katika uongeaji hata asietaka kusikia atakusikiliza!

Kutoa motisha. Hili nitalibeba kila ninapoteambea. Limekua ndio chachu ya jinsi tunavyoishi MCT hata katika nyakati ngumu!

Nitakukumbuka kwa umahiri wako katika uandishi na matumizi ya lugha.

Ni mengi mazuri ya kukusemea, itoshe kusema HONGERA SANA KWA UTUMISHI ULIOTUKUKA, natamani viatu vyako vinitoshe angali nikiwa kijana!

## Anna Nyoka:



Namuelezea vizuri kwa muda ambaye tumekaanaye kwa miaka 10 kama mfayakazi naye kama akiwa chifu ni mtu ambaye nimejifunza vitu vingi kutoka kwake. Ni mtu ambaye ni muelewa hata ukikosea kitu huwa anakuelekeza, anakuelewesha na hata kama mimi ndiyo namtengea chai kama katika chai sukari labda imezidi anakuambia "mama leo sukari imezidi kipimo" Baadaye, maisha yanaendelea. Nimekaa naye vizuri kwa miaka hiyo yote namuombea awe na maisha marefu nashurkuru kwa muda niliokaa naye. Ni kweli anajali maslahi ya wafanyakazi na ya kila kitu. Ni mtu mstaarabu na anayejali utu.

## Said Hassan Mloka



Alikuwa mvumilivu kwa wafanyakazi. Tunafanya makosa anaweza kuongea lakini yanaisha. Pia alikuwa anatetea maslahi ya wafanyakazi. Pakiwa na matatizo ya fedha anapambana ili mambo yawe sawa. Pili alikuwa ni mwalimu. Alikuwa mtu wa kukueleza. Kitu muhimu ninacho kumbuka ni msisitizo wa kuwa na diary itakayokuweza kutambua unachotakiwa kufanya kila siku husika.

Nimejifunza kutokana na utaratibu wa mpangokazi inayoonysha kila mtu anatakiwa afanye nini.

Work plan, quarterly plan na vikao vya mara kwa mara vimesaidia sana utendaji kazi.

Alikuwa akipigania waandish i-maslahi na haki zao za kisheria wakati mwingine mtu unaweza kufikiria kama vile anawadekeza.

Kwa mfano katika mikutano mikuu ya Baraza wajumbe wanalipiwa hoteli na fedha za kujikumu wakati katika taasisi zingine wajumbe hujilipia wenyewe kuhudhuria mikutano yao.

## Elizabeth Munisi



KM alikuwa ni zaidi ya bosi kwangu mimi. Amekuwa sawa na baba, mshauri wangu na rafiki. Maelekezo yake na kuniunga mkono, kumetengeneza dunia yangu. Ni heshima kubwa kufanya kazi chini ya uongozi wake. Amenifundisha mengi na mara zote nitamshukuru kwa kunipa nafasi hii. Ni kivutio cha kweli kwa kila mtumishi wa MCT. Jinsi anavyojitoa na moyo wake wa kuleta ufanisi, umeacha alama kubwa itakayodumu kwa muda mrefu kwa timu ya wafanyakazi wa MCT. Maelekezo yake na jinsi alivyoniunga mkono ni mambo yaliyonisaidia mimi kukua kibinafsi na kitaaluma. Ni heshima kuwa kuwa ni sehemu ya timu yake. Amesababisha maisha ya watu wengi wa MCT yawe na msimamo chanya katika kipindi cha uongozi wake kwenye Baraza na mchango wake kwenye timu ya MCT hautosahaulika. Ningependa kumshukuru kwa kila jambo alilonifanyia mini na watumishi wengine wa MCT na familia zao. Uongozi wake na maelekezo yake ni mambo yaliyosababisha mafanikio yetu. Kwa heri na kila la heri kwa ajili ya ukurasa mwingine wa maisha yake.

# Mazingira rafiki kwa wananahabari

*Inatoka Ukurasa wa 9*

ya Kupata Taarifa ya mwaka 2016, kwa kuwalazimisha watafuta taarifa kwenda TAMISEMI kupata barua ya kuwaruhusu kwenda kuomba taarifa katika halmashauri.

Matukio matano ya aina hiyo yamezihusisha halmashauri za wilaya za Mpwapwa, Muleba, Kilosa, Njombe na Halmashauri ya Mji wa Ifarakara ambapo katika tukio la Ifakara, ilibidi Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO) na Msemaji Mkuu wa Serikali kulitolea maelekezo.

Eneo jingine ambalo Baraza imekutana nalo mwaka huu, ni suala la Mkataba wa Bandari. Katika suala hilo Baraza limerekodi matukio yafuatayo, kunyimwa taarifa zilizohusiana na mkataba wa bandari tukio moja, vitisho matukio mawili na kukamatwa na baadaye kutakiwa kujieleza matukio mawili.

Matukio hayo pia yalihusu kukamatwa kwa waandishi ambao walirusha maoni ya kuupinga mkataba wa bandari, wengine walizuiwa kufanya kipindi kilicholenga kuujadili mkataba huo, na mwingine kutakiwa kujieleza polisi.

Katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Novemba mwaka huu, MCT kupitia kanzidata yake imerekodi madhila 21 ya waandishi wa kufanyiwa vitendo ama vinavyozuia kupata taarifa au vinavyofanya aogope kutimiza majukumu yake kama mwandishi wa habari.

Madhila hayo ni pamoja na kunyimwa taarifa matukio (8), vitisho (5), kukamatwa (3), mashambulizi (2), na udhalilishaji (3).

Mwaka huu matukio ya kunyimwa taarifa yamekuwa mengi zaidi ukilinganisha na miaka mitatu iliyopita, ambapo mwaka 2020 kulikuwa na matukio matatu, 2021 matukio manne na 2022 matukio mawili.

Kulingana huu kauli mbiu ya mwaka ya IDEI ni madhila dhidi ya waandishi wa habari, uadilifu wa uchaguzi, na jukumu la viongozi wa umma MCT imewakumbusha waandishi wa habari kuwa mwakani, Tanzania inaingia kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa, waandishi mnatakiwa kuwa makini katika uandishi wenu.

Imeeleza kuwa katika chaguzi zijazo kutakuwa na taarifa zinazoandaliwa na akili bandia, kutakuwa na habari zisizo kweli na pia kutakuwa hotuba za chuki ambapo Baraza limevitaka vyombo vya habari kujiandaa kutoa mafunzo kwa waandishi wake juu ya namna ya kugundua hizo aina mpya za upotoshaji



*Meneja wa Fedha wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), CPA Mustapha Tarimo akiwasilisha ripoti ya fedha katika Mkutano Mkuu wa Baraza uliofanyika Septemba 28,2023.*

# Mkutano Mkuu wapitisha mahesabu ya MCT

**Na Mwandishi wa Barazani**

Baraza la Habari Tanzania (MCT) limepata hati safi ya ukaguzi wa mahesabu yake kwa mwaka 2022.

Mahesabu hayo yalikaguliwa na kampuni ya ukaguzi ya Innovex Auditors.


Mahesabu hayo yaliyokaguliwa yalipitishwa rasmi na Mkutano Mkuu wa 25 wa Baraza uliofanyika Arusha, Septemba 28, 2023.

Ripoti iliyowasilishwa na Meneja wa Fedha wa Baraza, CPA Mustapha Tarimo imeeleza kwamba mwaka 2022, MCT ilitekeleza miradi kulingana na mpango mkakati wake wa 2018-2022 ambao haukufadhiliwa kwa ukamilifu.

Wafadhili wengi, CPA Tarimo alisema walikuwa wamebadili taratibu zao za ufadhili wakaamua kutoa fedha kwa sehemu moja ama zaidi ya mpango mkakati ambapo wengine walibadili maeneo ya vipaumbele vyao.

Hata hivyo, Baraza liliendelea kutafuta fedha kwa progranu zake mbalimbali kuhakikisha na kuwezesha malengo yake kutimia kwa kiasi kikubwa.

Katika hatua nyingine, Mkutano Mkuu uliiteua tena kampuni ya ukaguzi ya Innovex Auditors kukagua mahesabu ya MCT kwa mwaka unaomalizika Desemba 31, 2023 kufuatia mapendekezo ya Bodi.



*Mkurugenzi wa Idara ya Habari na Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi.*

# MAELEZO yakosoa taarifa ya kuzuia waandishi kutangaza habari za serikali

**Na Mwandishi wa Barazani**

Idara ya Habari (MAELEZO) na Ofisi ya Msemaji Mkuu wa Serikali imekosoa hatua ya kutoa katazo kwa wanahabari wa kujitegemea na vyombo binafsi iliyotolewa na ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji ya Ifakara Oktoba 9, 2023 kuwa siyo sahihi.

Taarifa iliyosainiwa na Mkurugenzi wa Idara ya Habari na Msemaji wa Serikali, Mobhare Holmes Matinyi iliyotolewa Oktoba 10, imeeleza Sheria ya Huduma ya Habari sura 229 kama ilivyofanyiwa marekebisho 2023 haikatazi wala kuzuia vyombo vya habari vya kujitegemea na waandishi wa kujitegemea kutoa taarifa za serikali isipokuwa kwa taarifa zilizozuiwa kwa mujibu wa sheria.

Kwa mujibu wa kifungu cha 7(i), sheria hiyo inaweka bayana haki za msingi za vyombo vya habari binafsi katika kutangaza masuala yenye umuhimu kwa taifa. Taarifa hiyo imeeleza kuwa kifungu cha 7(2),(b),(1V) kimeeleza wajibu wa vyombo vya habari vya binafsi kutangaza masuala yenye umuhimu kwa taifa na si katazo kwa vyombo hivyo kutoa taarifa, habari na matangazo ya serikali.

Idara ya Habari na Ofisi ya Msemaji Mkuu wa Serikali imetoa wito kwa vyombo vya habari na waandishi wa habari kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa uhuru na kutoa ushirikiano kwa serikali kwa kutangaza miradi ya maendeleo inayotekelezwa na serikali ya awamu ya sita na vile vile kuzingatia sheria, kanuni, weledi na maadili ya uandishi wa habari.

Baada ya kutolewa taarifa hii, siku iliyofuata Oktoba 11, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji ya Ifakara, Lena M. Nkaya aliomba radhi kutokana na taarifa iliyotolewa na mtumishi wake Oktoba 9 na kusambazwa katika mitandao ya kijamii ikitoa katazo kwa vyombo vya habari vya kujitegetemea na waandishi wa habari kutoa habari na matangazo yanayohusu serikali.

Mkurugenzi huyo alisema huo siyo msimamo wa Halmashauri kwa kuwa kufanya hivyo itakuwa kukiuka haki ya uhuru wa habari na uhuru wa kujieleza.



Mjumbe kutoka Zanzibar, Jabir Idris, akizungumza katika Mkutano Mkuu wa MCT, mjini Arusha Septemba 28, 2023.

# Kutolipa ada ya uanachama MCT kwazua mjadala

**Na Tumbi Kiganja**

Tatizo sugu la kutolipa ada ya uanachama lilibua mjadala mkubwa katika Mkutano Mkuu wa 25 wa Baraza la Habari Tanzania uliofanyika mjini Arusha 28 Septemba 2023.

Akiwasilisha sehemu ya ripoti ya Katibu Mtndaji wa Baraza, Meneja wa Fedha CPA Mustapha Tarimo alisema michango ya wanachama iliyokusanywa kwa mwaka ni sh. 9,300,000 ambacho ni kiasi kidogo ikilinganishwa na idadi kubwa ya wanachama.

Kama wanachama wote 243 wangelipa ada zao, alisema CPA Mustapha kiasi kilichokusanywa kingekuwa karibu sh. 40,000,000. Wanachama wapya 12 wamejiunga na Baraza mwaka huu.

Kuibuka kwa taarifa hizi, kulizua mjadala huku baadhi ya wajumbe wa mkutano wakiitaka Sekretariati ya Baraza kuzungumza na wanachama wenye madeni makubwa ya ada kuona jinsi watakavyoyapunguza na kulipa.

Baraza pia lilishauriwa kuangalia kwa makini kama wanachama walioorodheshwa kama wadaiwa sugu kama kweli bado hai.

Akizungumzia suala hilo, Katibu Mtendaji, Kajubi Mukajanga , alisema wanachama wenye madeni makubwa wapo na ndiyo wanufaika wakubwa wa huduma za Baraza lakini hawalipi ada zao.

Alisema Sekretariati imekuwa ikiwakumbusha wanachama kulipa ada zao kila ifikapo Januari mosi kila mwaka.

Akitolea mfano usemi kwamba hakuna bonasi bila wajibu, Mukajanga alisema ni jukumu la Mkutano Mkuu kuamua hatua za kuwachukulia wanachama wasiolipa ada zao baada ya kupokea mapendekezo ya Bodi ya Baraza.

Hata hivyo alisema yeye kama Katibu wa Bodi, asingependa kuchukuliwa kwa hatua kali kama kuwafuta uanachama wadaiwa.

Rais wa Baraza Jaji mstaafu Juxon Mlay akiongoza kikao hicho kwa njia ya mtandao akiwa Mumbai, India aliwasihi wanachama kuzingatia wajibu wao wa kulipa ada zao.

Alisema Baraza ni lao na wawe na dhamira nalo.

Masuala mengine yaliyoibuka wakati wa majadiliano ya ripoti ya Katibu Mtendaji ni pamoja na vichwa vya habari vinavyohukumu na utangazaji ambao ulielezwa kama 'porojo', hasa katika radio za FM.

Kuhusu vichwa vya habari vinavyohukumu, Ofisa Programu Paul Mallimbo alisema kwa kawaida Baraza huwasiliana na wahariri kila inapotokea kichwa cha habari cha aina hiyo na kuwaeleza kuwa jukumu la kuhukumu ni la mahakama na siyo la vyombo vya habari.

Vilevile Baraza pia huwasiliana na radio za FM na kuhimiza waachane na porojo katika matangazo yao.

Kuhusu matangazo mubashara ya Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT), Mallimbo alisema Baraza huwaandikia vituo vingi likiomba vifanye matangazo mubashara ya tuzo hizo. Baadhi , alisema, hujibu na vingine hukaa kimya.

Ofisa Programu mwingine wa Baraza Saumu Mwalimu, akizungumzia suala la maofisa wa MCT kutembelea wanachama wa Baraza walio maeneo ya pembezoni, alisema kuwa mara nyingi maofisa wa Baraza wanapokuwa na shughuli mikoani hutumia nafasi hiyo kutembelea wanachama wao.

Alisema wamezingatia suala hilo na kwamba watatimiza takwa hilo kila itakapotokea fursa.



*Wajumbe mbalimbali ambao ni wadau wa tasnia ya habari wakiwemo Baraza la Habari Tanzania (MCT) wakiwa katika kikao cha Kamati iliyoundwa na Serikali Kutathmini hali ya uchumi wa vyombo vya Habari nchini. Kikao hicho kilifanyika Novemba 3, 2023 kwenye ukumbi wa mikutano wa Idara ya Habari (MAELEZO) uliopo jengo la TTCL Extelecoms- Dar es Salaam.*

# MCT yashiriki kutathmini hali ya uchumi ya vyombo vya habari

**Na Mwandishi wa barazani**

Mapema mwanzoni mwa mwaka huu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara yake ya Habari, Mawasiliano na Tekinolojia ya Habari iliunda kamati ya kutathmini hali ya uchumi wa vyombo vya habari nchini

Moja ya majukumu ya Kamati hiyo ilikuwa ni kukutana na wadau mbalimbali wa habari na kupata maoni yao juu ya mambo kadhaa yanayoikabili tasnia ya habari.

Novemba 3, 2023 Baraza la Habari Tanzania (MCT) lilipata nafasi ya kutoa maoni yake kwa kamati hiyo. MCT iliwakilishwa na maafisa wake wawili, Paul Mallimbo na Tumbi Kiganja ambapo pamoja na mambo mengine maafisa hao waliileza kamati hiyo hali ya waandishi wa habari na watumishi wengine wasiokuwa waandishi wa habari kuhusu vipato vyao, mikataba ya kazi, elimu na mazingira ya kazi.

Vilevile, MCT ilielezea kamati hiyo kuhusu hali nzima ya vyombo vya habari kiuchumi na utendaji nchini pamoja na sababu zinazoleta changamoto hizo za kiuchumi katika vyombo vya habari na kushauri juu ya namna bora ya kufanya ili kukabiliana na changamoto hizo.

Pamoja na MCT, taasisi nyingine zilizopata nafasi ya kutoa maoni siku hiyo ni pamoja na Mtandao wa Redio za Kijamii Tanzania (TADIO), Muungano wa Klabu za Habari Tanzania (UTPC) na Chama Cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA)

Awali, wakati wajumbe wakichangia walisema kuwa hali ya matatizo ya kiuchumi yalianza muda mrefu lakini ilipofika mwaka 2015 hali hiyo ilizidi kuwa mbaya ikichangiwa na upepo wa kisiasa kwa kipindi hicho.

Utawala ulioingia madarakani uliweka mbinyo wa uhuru wa kujieleza hali iliyofanya baadhi ya waandishi na vyombo kushindwa kuandika habari za kiuchunguzi kwa kuogopa mkono wa dola. Mathalani, waandishi na wahariri kadhaa walikuwa wakiitwa na mamlaka kuhojiwa mara kwa mara kutokana na habari ambazo zilikuwa zikichapishwa au kutangazwa kwenye vyombo vyao.

Habari za uchunguzi zilipungua kwa kiasi kikubwa huku waandishi na vyombo vyao wakijikita zaidi katika habari za matukio kama vile semina, vikao na matamasha.

Aidha, utawala uliokuwepo kwa kipindi hicho uliamua kupeleka matangazo yake kwa vyombo vya habari vya serikali pekee huku wakiviacha vile vya binafsi vikihaha kujiendesha kwa kuwa ni ukweli ulio wazi kuwa vyombo vingi vimekuwa vikijiendesha kwa kutegemea matangazo zaidi na pia Serikali ndio imekuwa mtangazaji mkuu kwa hapa nchini. Hali hii ilipelekea baadhi ya vyombo vya habari kusuasua na vingine kufa huku vikiacha waandishi na watumishi wake kukosa ajira na wakiendelea kuvidai vyombo hizo.



Mshindi wa Tuzo ya Mafanikio ya Maisha katika Uandishi wa Habari na Jaji wa EJAT 2022, 2022, Rose Haji (kushoto) akifuatilia majadiliano wakati wa mafunzo maalum ya EJAT yaliyofanyika Dodoma kuanzia Novemba 13 – 14, 2023.

# Andikeni habari za jamii – Mukajanga

Na Tumbi Kiganja, Dodoma

Waandishi wa habari nchini wametakiwa kuandaa kazi zenye ubora na za kiushindani kwa kuzingatia weledi wa kitaaluma kwa ajili ya jamii.

Haya yamesemwa jijini Dodoma na Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT) Kajubi Mukajanga, wakati akifungua mafunzo maalumu ya siku tatu -EJAT Master Class - yaliyofanyika kama sehemu ya kutoa mrejesho wa kazi zilizotumwa kwa ajili ya kushindanishwa katika Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT)

Mukajanga alisema kuwa lengo la mafunzo haya ni kukumbushana namna ya kuandaa habari za kila siku kwenye vyombo vyetu vya habari lakini pia vipindi hivi viweze kuletwa kwenye tuzo za EJAT.

"Baadhi ya waandishi wamekuwa na mtazamo wa kuandaa vipindi na makala kwa ajili ya EJAT tu kitu ambacho sio sahihi. Andaeni vipindi na makala kwa ajili ya vyombo vyenu ili pia siku unapotaka kushiriki tuzo basi unachagua makala au kipindi chochote na kuleta kwenye mashindano," aliongeza Mukajanga.

Mafunzo haya yaliandaliwa na MCT ikishirikiana na Ofisi ya Kamishina Mkuu wa Haki za Binadamu - Ofisi ya Afrika Mashariki (OHCHR- EARO), ambapo mtaalamu wa masuala ya haki za binadamu toka Ofisi hiyo, Catherine Njuguna alisema kuwa haki za binadamu ni msingi wa maisha kwa kila binadamu

"Ninyi waandishi wa habari mmekuwa nguzo muhimu sana katika kubeba agenda mbalimbali kwenda kwa jamii husika. Sisi (OHCHR- EARO) tumeona umuhimu wa kufanya kazi na waandishi wa habari hapa Tanzania na ndiyo maana tumekuwa tukifanya mafunzo haya kwa pamoja na MCT. Habari zenu za kila siku zimekuwa zikigusa eneo nyeti la haki za binadamu hasa katika maeneo ya habari za Watoto, Uchunguzi, Elimu, Jinsia nakadhalika"

Mafunzo haya pia yalihusisha majaji wawili wa EJAT ambao ni Dk. Egbert Mkoko, mhadhiri kutoka Chuo kikuu cha Dar es Salaam na Bi. Rose Haji Mwalimu mwandishi na mtangazaji wa siku nyingi ambaye pia ni mshindi wa Tuzo ya Mafanikio ya Maisha (LAJA) 2016.

Kwa upande wa majaji walielezea vigezo mbalimbali ambavyo wamekuwa wakivitumia wakati wa kupitia kazi zinazowasilishwa kwa ajili ya tuzo.

Aidha Dk. Mkoko alifundisha mada kadhaa zikiwemo namna ya kufanya habari za uchunguzi, mbinu na namna ya kufanya mahojiano lakini pia aliwafundisha washiriki hao kuhusu sababu mbalimbali zinazofanya baadhi ya kazi zinazoletwa kwenye tuzo kutofanya vizuri.

Dk. Mkoko alisema kuwa baadhi ya washiriki wamekuwa wakileta kazi ambazo zina mawazo mazuri sana lakini wanashindwa kuzitendea haki kwa kukosea baadhi ya vitu muhimu.

"Kazi nyingi zinazoletwa kwenye mashindano zimekuwa na changamoto za kimaadili, matumizi mabaya ya lugha, zingine hazina upekee, kutojikita katika wazo kuu, hazina ubunifu, hakuna utafiti wa kina lakini pia ukosefu wa takwimu toka kwa vyanzo sahihi," alisema mhadhiri huyo.

Rose Haji alifundisha mbinu za kuandaa makala au vipindi vya redio na runinga vyenye uwezo wa kuvutia wasomaji, wasikilizaji na watazamaji. Alisema kuwa bado kuna shida ya matumizi ya lugha hasa kwenye kutamka baadhi ya maneno ya Kiswahili, pia matumizi ya lugha ya picha.

Endelea Ukurasa wa 20

# Andikeni habari za jamii – Mukajanga

*Inatoka Ukurasa wa 19*

"Sasa hivi ukisikiliza redio kwa kweli unaweza hisi kichefuchefu maana lugha zinazotumika si rafiki, matamshi ya maneno yanakosewa, mathalani utasikia mtangazaji anasema kuwa leo hapa studio niko na wamama wawili na wababa watatu…. haya sio matumizi sahihi ya lugha," alionya Rose Haji.

Baadhi ya washiriki waliohudhuria mafunzo hayo walitoa maoni yao kwa kusema kuwa mafunzo haya yamewapa mwanga wa kujua ni namna gani wanapaswa kuandaa vipindi vyao na hata vile vya kupeleka kwenye EJAT basi viwe vya namna gani.

Lisungu Kambona kutoka ZCTV na Hits FM alisema kuwa yeye awali alikuwa akilalamika sana kuona kuwa anajitahidi kushiriki kwenye EJAT zaidi ya mara tatu mfululizo lakini hajawahi hata kutajwa jina lake na alikuwa akiamini kuwa kuna upendeleo wa wale wanaoteuliwa na kushinda.

"Naomba leo niombe radhi kwa imani ambayo nilikuwa nayo awali, kwa darasa hili la siku tatu basi naona kwa kweli zile kazi zangu hazikuwa na ubora wa kushindanishwa," alisema Lisungu

Maryline Olotu kutoka redio ya kidini ya Kilimanjaro Revival alisema kuwa yeye hajawahi kushiriki tuzo lakini kwa elimu aliyoipata anaamini kuwa yeye atakuwa mmoja wa washindi wa EJAT 2023.

"Nilikuwa pia nikisikia malalamiko ya baadhi ya waandishi wenzangu wakiamini kuwa EJAT ni kwa ajili ya baadhi ya waandishi na vyombo fulani, lakini hapa nimeona mambo yalivyo wazi ni vigezo ndivyo vinaamua mshindi."

Baada ya mafunzo, washiriki pia waliwekwa kwenye makundi manne (redio, runinga, magazeti na vyombo vya habari vya mtandaoni) kisha kupewa mifano ya kazi ambazo ziliwahi kutumwa kushindanishwa kwenye EJAT na wakatakiwa kuzisoma, kusikiliza na kuangalia na wazifanyie maamuzi kama majaji kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa.

Pamoja na mafunzo ya EJAT, washiriki pia walipata nafasi ya kufundishwa kuhusu umuhimu na misingi ya Azimio la Dar es Salaam Juu ya Uhuru wa Uhariri na Uwajibikaji - DEFIR,

Ally Ngamba kutoka Uyui FM ya Tabora alisema mafunzo haya yamekuwa na tija kubwa sana kwa Waandishi ambao wameshiriki kwani yamewatengenezea mwanga wa namna gani ya kutengeneza vipindi bora kwa ajili ya vituo vyao na pia kwa ajili ya mashindano ya EJAT.

Pia yamewasaidia washiriki kutengeneza umoja ambao utawasaidia kujadiliana masuala mbalimbali yanayohusu tasnia ya habari ikiwemo tuzo za EJAT.

Mafunzo haya yalifanyika Morena hoteli jijini Dodoma na yalihusisha waandishi ya 28 ambao walitoka kwenye vyombo mbalimbali vya habari ikiwemo redio, runinga, magazeti na vyombo vya habari vya mitandaoni. Washiriki hao walitoka katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Dodoma, Shinyanga, Tabora na Iringa. Wengine walitoka Pemba, Tanga, Geita, Lindi na Kagera.



*Jaji wa EJAT 2022 Dk. Egbert Mkoko akitoa mafunzo kwa waandishi kuhusu mambo yanayoua habari za kushinda tuzo katika mafunzo maalum ya EJAT yaliyifanyika Dodoma kuanzia Novemba13 – 15, 2023.*



Wadau wa habari wakishiriki mkutano wa kujadili marekebisho ya Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari.

# Wadau waendelee kuelimishwa, wajihadhari na vifungu vya MSA 2016 visivyo rafiki

Na Saumu Mwalimu

Wadau na taasisi za habari waendelee kutoa elimu kuhusu mapungufu yaliyopo kwenye sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari, 2016 kwa sababu bado ina mapungufu mengi.

Mwezi Juni, 2023 Bunge lilipitisha marekebisho ya sheria hiyo yaliyoletwa kwa njia ya muswada wa Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali, 2023. Katika mabadiliko hayo, vifungu vinane tu kati ya 21 vilivyopendekezwa na wadau vilifanyiwa marekebisho.

Wakizungumza wakati wa mkutano wa siku moja uliofanyika Novemba 3, 2023 jijini Dar es Salaam kujadili mabadiliko hayo katika Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari, 2016 wadau wa habari wametahadharisha kwamba, sheria hiyo bado ina meno makali katika mustakabali wa sekta ya habari.

Walionya kwamba, wakati nchi ikielekea katika chaguzi mwaka 2024 na 2025 vipo vifungu ambavyo vinabama ufanyaji kazi wa uhuru wa waandishi na vyombo vya habari.

Kwa mfano kifungu cha 7(2) b (iv) kinatoa maelekezo kwa vyombo vya habari binafsi kuchapisha habari zenye umuhimu kwa taifa kwa maelekezo ya Serikali, "... kama serikali itakavyoagiza."

Na kifungu cha 52(1)d kinahusu masuala ya nia ya uchochezi bila kutoa tafsiri ya uchochezi ni nini wala kuelezea nini kinahusika kwenye uchochezi, hivyo kutoa mwanya wa makundi ya mamlaka mbalimbali kukitumia vibaya kifungu hiki kwa sababu dhana na maana ya uchochezi vimeachwa kwenye utashi wa mtu. Kifungu hiki kina hatari ya kuminya uhuru wa kujieleza na kutoa maoni.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mkutano huo Mkurugenzi wa Misa-Tan Elizabeth Riziki alisema kwamba lengo la mkutano huo lilikuwa ni kujadili mambo kadhaa ya kufanya baada ya marekebisho ya sheria hiyo ili kuhakikisha waandishi wa habari, vyombo vya habari pamoja na wananchi wanafurahia uhuru wao wa kihabari na kujieleza.

*Endelea Ukurasa wa 22*

# Wadau waendelee kuelimishwa, wajihadhari na vifungu vya MSA 2016 visivyo rafiki

*Inatoka Ukurasa wa 21*

"Misa-Tan kwa kushirikiana na wadau wetu Protection International Africa tunatakeleza mradi ambao pamoja na malengo mengine ni kutetea uhuru wa habari kwa kuhakikisha mazingira ya kisheria yanakuwa bora," alisema.

Kwa upande wake Mhariri wa gazeti la Mwananchi Lilian Timbuka alisema kwamba wakati taifa likielekea kwenye vipindi cha uchaguzi, ni muhimu waandishi na vyombo vya habari vikajuzwa ni kwa kiasi gani mabadiliko yaliyofanyika kwenye sheria yameleta nafuu katika utendaji kazi wao na zipi ni changamoto.

"Labda niulize, unafuu ulioletwa na mabadiliko haya ni wa kiasi gani kwa sababu mwakani (2024) na 2025 tunaingia katika chaguzi, yapi tuyatarajie ili tusijikute katika mikono ya sheria?" aliuliza Lilian Timbuka.

Akitoa ufafanuzi juu ya swali hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Taarifa kwa Wananchi (TCIB), Deus Kibamba alisema ni muhimu vyombo vya habari kuzingatia miongozi ya kuripoti uchaguzi inayotolewa na Tume ya Uchaguzi pamoja na TAMISEMI.

Wakati huo huo Ofisa Programu wa Media Council of Tanzania (MCT) Saumu Mwalimu akisisitiza MCT inao mwongozo kuhusu kuandika habari za uchaguzi lakini 'Media Codes of Conduct for Election Reporting' pia kuna kanuni za maadili ambazo ndio msingi katika uandishi wa habari za aina yoyote.

"Sio kipindi cha uchaguzi tu, kuzingatia maadili ni kwa wakati wote, lakini inapofika katika vipindi vya uchaguzi muhimu tuisome na tuzingatie miongozi kuhusu uandishi wa habari za uchaguzi, mwongozo uliotolewa na MCT upo kwenye tovuti yake ya www.mct.or.tz," alisema Saumu Mwalimu akiongeza umuhimu wa waandishi kuyafahamu mabadiliko haya MSA 2016.



*Ofisa Programu wa Baraza la Habari Tanzania, Saumu Mwalimu akizungumza katika mkutano wa wadau kujadili marekebisho ya Sheria ya Huduma ya Habari.*